JIFUNZENI HIGH SCHOOL
S.L.P. 6209, MBEYA
Email: jssp2008@yahoo.com

JIFUNZENI IN SOCIAL SERVICES PROMOTION (JSSP)
Jifunzeni High School
P.O. BOX 6209
MBEYA – TANZANIA
Cell: 0754645975/0754543934.E- mail:jifunzenisecondary@gmail.com
Website: www.jifunzenischools.ac.tz

**REF NO: JSSP/JSS/JI/VOL 02/025/001**

**MZAZI /MLEZI WA ..........................................................................................**

## FOMU YA KUJIUNGA KIDATO CHA V/VI

## YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA .......... MWAKA 2025/2026

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Uongozi wa shule ya sekondari ya Jifunzeni unakushukuru na kukupongeza kwa kuthubutu na kupenda mwanao kuwa miongoni mwa wanafunzi walioomba kusoma kidato cha **V/VI** Mwaka wa masomo 2025

Baada ya kukidhi vigezo vilivyo wekwa, uongozi wa shule unayofuraha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha **V/VI** katika mchepuo wa **HGL( ),HKL( )** na **HGK(),EGM ( ), HGE ( ),ECA( ),PCM ( ), PCB ( ), CBG ( ), PGM ( )** weka alamaya vema (√) kwenye braketi ndio mchepuo uliochagua kusoma katika shule yetu.

Masomo yataanza tarehe **.........................saa 1:30** asubuhi kwa wanafunzi wote. Wanafunzi wa bweni wanatakiwa kufika shuleni tarehe**......................**mwisho kuwasili ni saa **nane mchana** (8:00) kwa maandalizi ya siku ijayo. Kumbuka nafasi uliyopata ni ya pekee hivyo epuka nafasi yako kujazwa na wengine kwa kutokuwepo shuleni siku uliyoelekezwa/agizwa kufika .

Tunaambatanisha barua hii na:-

- **i)** Fomu ya maelezo ya kujiunga na shule
- **ii)** Sheria za shule

**Tunatanguliza shukrani, karibu Jifunzeni High School.**

**....................................................**

**MKUU WA SHULE**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NAJIFUNZENI HIGH SCHOOL KIDATO CHA ………………. MWAKA 2025**

1. **SHULE ILIPO:**
   Shule ipo mkoa wa Mbeya katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kata ya Ilomba mtaa wa Ituha. Ipo umbali wa km 2 kutoka kituo cha mabasi Ituha.

2. **MASOMO YANAYOFUNDISHWA:**
   - i) HISTORY
   - ii) GEOGRAPHY
   - iii) ENGLISH
   - iv) KISWAHILI
   - v) GENERAL STUDY
   - vi) Biology
   - vii) Chemistry
   - viii) Physics
   - ix) Advanced Mathematics
   - x) Basic Applied Mathematics
   - xi) Commerce
   - xii) Economics
   - xiii) Accounts

Masomo hayanikwa msingi wa michepuo ya **HGL, HGK**,**HKL,HGE, EGM, ECA, CBG, PCM, PCB NA PGM**

NB:-Lugha ya kufundishia ni kiingereza kwa masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili

## 3. VITABU

Aje na vitabu kuzingatia mchepuo atakao soma ili kujiimarisha zaidi na kujisomea binafsi. Kwa masomo ya sayansi aje na scientific calculator.

| **SOMO** | **KITABU** |
|---|---|
| Biology | Biological science, New Understanding Biology |
| chemistry | Conceptual of chemistry class XI,XII |
| Physics | Principles of physics XI,XII |
| Basic applied mathematics(BAM) | TIE |
| General studies | General studies alive by Zisti |
| Geography | Practical geography alive, Geography II alive by Zisti Kamili |
| History | Essential in advanced history 01&02 by Salehe Yassin |
| Kiswahili | Nadharia ya Lugha na Tahakiki, waandishi ni Masebo na Nyangwine |
| English language | Comprehensive Linguistics 5&6 by mgonja, Advanced level literature by Godfrey bukagire |
| Economics | Essential of Economics 01&02 |
| Accounts | Frank Wood vol.01&02 |
| Commerce | Textbook of commerce vol.01& 02 |

| | |
|---|---|
| Advanced mathematics | Advanced mathematics for advanced secondary schools form V&VI |

## 4. SARE YA SHULE

**Vifaa vinavyotakiwa kwa wanafunzi wa Hosteli.Kila mwanafunzi aje na :**

## A: WAVULANA

**VIFAA VINAVYOPATIKANA SHULENI**

**i)** Suruali mbili rangi nyeusi na suruali mbili rangi ya bluu nyeusi(dark bluu), zinapatikana shuleni kwa **sh, 40,000@ =** **160,000/=**

**ii)** Sweta rangi ya **bluu-nyeusi** zinapatikana shuleni kwa sh**. 20,000**/= jumla sh **20,000/=**

**iii)** T-shirt mbili zinapatikana shuleni kwa sh. **20,000** kila moja = jumla **40,000/=**

**iv)** Kitambulisho sh. **10,000** = jumla Tshs **10,000/=**

**JUMLA 230,000/**

**VIFAA VITAKAVYO NUNULIWA NYUMBANI**

i. Mkanda mweusi
ii. Tai nyeusi jozi moja
iii. Shati mbili rangi nyeupe mikono mirefu
iv. **SHAMBA TROUSER (SURUALI) RANGI DAMU YA MZEE**
v. Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili (2) vinavyofunika miguu na kisigino kifupivyenye kamba
vi. Soksi jozi mbili rangi nyeusi
vii. Aje na picha tatu passport size
viii. Godoro upana **FT** $2^{1}/_{2}$ na urefu **FT 6**
ix. Blanketi zitomoja .
x. Mashuka mawili rangi ya bluu bahari.
xi. Mto na foronya.
xii. Taulo moja sanduku la chuma.
xiii. Ndala (kanda mbili).
xiv. Ndoo ya maji ndogo
xv. Jembe lenye mpini aina ya chapakazi, fagio aina ya chelewa
xvi. Kwanja (fyekeo)
xvii. Tracksuti rangi nyeusi yenye ufito mweupe.
xviii. Sare ya michezo, raba au viatu vya michezo
xix. Mswaki, dawa ya meno, kiwi, Mafuta ya Kupaka, Sabuni za Kufuria na Kuogea, Toilet Paper na Chandarua (Net).

## B: WASICHANA

**VIFAA VINAVYOPATIKANA SHULENI**

i. Sketi mbili rangi  nyeusina sketi  2 rangi ya bluu nyeusi(dark bluu) ndefu kupita magoti mshono wa malinda zinapatikana shuleni kwa sh  **35,000** kila moja = **140,000/=** mashono ya nyumbani hayatakubalika.
ii. Sweta rangi ya **bluu-nyeusi** zinapatikana shuleni kwa  sh**. 20,000**/= jumla  sh **20,000/=**
iii. T-shirt mbili zinapatikana shuleni kwa sh. **20,000** kila moja = jumla **40,000/=**
iv. Kitambulisho sh.  **10,000** aje na picha tatu passport size = jumla Tshs **10,000**/=

**Jumla ni Tsh. <u>210,000/=</u>**

**<u>VIFAA VITAKAVYO NUNULIWA NYUMBANI</u>**

i. Shati mbili rangi nyeupe mikono mirefu aje nazo.
ii. Tai nyeusi jozi moja
iii. **SHAMBA DRESS RANGI DAMU YA MZEE (GAUNI REFU MASHONO SOLO )**
iv. Soksi jozi mbili rangi nyeupe aje nazo.
v. Viatu vya ngozirangi  nyeusijozi mbili (2)  kisigino kifupi vinavyofunika miguu vyenye kamba.
vi. Godoro upana **FT** $2\frac{1}{2}$na urefu **FT 6**
vii. Blanketi  zito moja .
viii. Mashuka mawili rangi ya Pinki.
ix. Mto na foronya.
x. Taulo moja sanduku la chuma.
xi. Ndala (kanda mbili).
xii. Aje na picha tatu passport size
xiii. Ndoo ya maji ndogo
xiv. Brashi ya kusugulia choo( short brush) skuiza na fagio la chelewa.
xv. Tracksuti rangi bluu bahari yenye ufito mweupe.
xvi. Sare ya michezo, raba au viatu vya michezo
xvii. Mswaki, dawa ya meno, kiwi, Mafuta ya Kupaka, Sabuni za Kufuria na Kuogea, Toilet Paper na Chandarua (Net).

## C: CHAKULA

Aje na kontena la chakula lenye mfuniko, kijiko na kikombe. Hakutakuwa na chakula maalum (**special diet**) kwa mwanafunzi.yeyoye

## D: ILANI:

Shule ni ya hosteli, hivyo Mwanafunzi haruhusiwi kuondoka bwenini na kwenda kulala njeya maeneo ya shule pasipo ruksa ya mkuu wa shule.

JSSP
S.L.P 6209, MBEYA
EDUCATION FOR ACHIEVEMENTS

## 5.ADA YA SHULE

Ada kwa mwanafunzi itakuwa :

| | | |
|---|---|---|
| i. | Ada ya Shule ni | 800,000/= |
| ii. | Ada ya Hosteli ni Tshs | 1,100,000/= |
| | **JUMLA NI TSHS** | **1,900,000/=** |

**Nayo italipwa kama ifuatavyo:-**

JSSP
S.L.P. 6209, MBEYA
EDUCATION FOR ACHIEVEMENTS

### ADA YA MWANAFUNZI WA KUTWA (DAY)

**May 2025** - shule inapofunguliwa Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha **SH. 300,000/=**

**SEP2025** - shule inapofunguliwa Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha **SH. 200,000/=**

**JAN2026** - shule inapofunguliwa Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha **SH. 200,000/=**

**March/April2026** - shule inapofunguliwa Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha **SH. 100,000/=**

**JUMLA NI TSHS 800,000/=**

### ADA YA MWANAFUNZI WA BWENI (HOSTELI)

**May2025**- shule inapofunguliwa Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha **SH.600,000/=**

**Sept 2025** - Baada yamid -tem Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasicha **SH. 400,000/=**

**January 2026**-Shule inapofunguliwa Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha**SH.500,000/=**

**March/April –2026** Baada ya mid-tem Mwanafunzi aje na risiti yenye malipo ya kiasi cha **SH.400,000/=**

**JUMLA NI TSHS. 1,900,000/**

### MASHARTI YA ULIPAJI

Mzazi unaombwa kulipa malipo yote ya ada ya shule na Hosteli katika Benki na kuwasilisha risiti ya benki (**Pay in-slip**) ili ukatiwe risiti ya ada Kwa akaunti zifuatazo:-

i) NMB - Jina la akaunti - JIFUNZENI SECONDARY SCHOOL
**Akaunti Namba (62506600004)**

ii) CRDB-Jina la akaunti - JIFUNZENI SECONDARY SCHOOL
**Akaunti Namba (0150422064900 )**

Risit ya Benki (***Pay in-slip*** ) iwasilishwe shuleni mara  anapowasili mwanafunzi bila kukosa, Kumbuka kuandika jina na kidato cha  Mwanafunzi kwenye risiti na namba ya simu ya mzazi.

## *ANGALIZO*

***Tafadhali : hatutapokea pesa Tasilimu (Cash)***

***Epuka kuagizia fedha kwa mtu yeyote wala kutumia M-Pesa, zingatia maelekezo ya hapo juu.***

***ADA IKILIPWA HAIRUDISHWI***

## 6. MENGINEYO

i) Kuimarisha taaluma kila mwanafunzianatakiwa kuleta **Rimu** nne (4) ya karatasi aina ya **A4**. Mbili muhura wa I na nyingine iletwe  muhula wa II
ii) **Mwanafunzi aje na Bima ya Afya.**
iii) Aje na daftari  kumi (10) aina ya Counter Books zenye 3 quire kwa ajili  ya masomo.
iv) Alete picha za wazazi /walezi moja kwa kila mzazi/ mlezi (passportsize) na mtoto picha tatu.
v) Pia mwanafunzi aje na**spring file**moja kwa ajili ya kutunza taarifa mbalimbali za mwanafunzi na pili aje na box file kwa ajili ya kutunza mitihani yake.
vi) Vilevile aje na mkebe (**Mathematical set**) kwa ajili ya Geography
vii) Ambatanisha copy ya result slip ya mtihani wa taifa kidato cha nne.
viii) **Hakikisha mwanafunzi anakuja na bima ya afya**

**UONGOZI WA JIFUNZENI HIGH SCHOOL UNAKUTAKIA UTEKELEZAJI MWEMA WA MAAGIZO YOTE.**

***MOTO WA SHULE: - "EDUCATION FOR ACHIEVEMENT"***

**Pamoja na maelekezo ya kujiunga naambatanisha na sheria za shule, zisome kwa makini na uzielewe kisha mwishoni mwa ukurasa mzazi andikajina na sahihi na mtoto jina na sahihi. Utakapo mleta mtoto hakikisha unakuja na hiyo nakala ya sheria uliyosaini wewe na mtoto.**

# SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule ya JifunzeniHigh School inalenga kuwajenga, kuwalea na kuwaongoza katika maadili na misingi bora ya kikristo. Hivyo basi:-

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia, kuheshimu, kuhudhuria na kufuata ratiba na taratibu zote za ibada zitakazoendeshwa shuleni. ***KUTOKUFANYA HIVYO MWANAFUNZI AWEZA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA***.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa aishi kwa amani/utulivu, heshimana upendo. Lazima aheshimu walimu wote pamoja na wafanyakazi wasio walimu ikiwa ni pamoja na wanafunzi wenzake waliopo shuleni. Kwa sababu hiyo ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kupiga, kupigana, kutukana, kuanzisha au kushiriki vurugu ya aina yoyote iwayo. Kwa kufanya hivyo ***MWANAFUNZI AWEZA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.***
3. Ni mwiko kabisa mwanafunzi kufanya:- mapenzi, uasherati, kuoa au kuolewa, kubaka, kunajisi, kulawiti, kutoa mimba, kusababisha mimba, utoro, kutumia madawa ya kulevya, kuingia kwenye vilabu vya pombe, baa, nyumba za kulala wageni au kumbi za starehe, kupuuza wimbo wa Taifa au kutoheshimu na kuchana bendera ya Taifa. ***IKITHIBITIKA ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA***
4. Kutohudhuria vipindi kama ratiba ya shule inavyoonesha, yaani kutoroka shule au kuonekana bwenini muda wa darasani bila kibali chochote adhabu kali itatolewa kwa mwanafunzi husika.
5. Ni marufuku mwanafunzi kuvuta sigara, bangi na tumbaku.
6. Ni marufuku mwanafunzi yeyote kuendesha shughuli za kisiasa na biashara shuleni.
7. Ni marufuku mwanafunzi yeyote kupiga kelele, kufanya fujo na kuzomea
8. Kila mwanafunzi analazimika kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika:-
   a) Maongezi na walezi wake pasipo kutumia lugha chafu
   b) Lugha ya mitaani, kubishana, kukebei au kuguna
   c) Kila mwanafunzi analazimika kusimama na kusalimia mwalimu/mfanya kazi asiye mwalimu/mtu yeyote aliye mzidi umri apitapo au kuingia mahali popote la sivyo ***ATAKABILIWA NA ADHABU KALI.***
9. Matatizo yote ya shule lazima yatatuliwe kwa kutumia kanuni na taratibu za shule hii. Hivyo ni kosa kwa mwanafunzi kupeleka malalamiko nje ya shule moja kwa moja.
10. Mwanafunzi haruhusiwi kushtaki au kushtakiwa mahakamani, pindi mwanafunzi akifika au kufikishwa mahakamani kwa mashtaka ya aina yoyote ile ***ATASIMAMISHWA MASOMO MARA MOJA.***
11. Ni wajibu wa kila mwanafunzikutunza mazingira, majengo, samani na mali za shule, kinyume chake ***MWANAFUNZI ATAKABILIWA NA ADHABU YA KUMTOSHA.***
12. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria na kutii wito wowote kama vile baraza la shule, morning parade, afternoon parade,michezo, roll call na mikutano mingineitakayoitishwa na uongozi wa shule.
13. Kila mwanafunzi anatakiwa awe kwenye sare ya shule wakati wowote awapo shuleni na anapotoka nje ya mipaka ya shule na kuwa msafi muda wote.
14. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya anatakiwa kuonesha cheti kuhusiana na tatizo lake mara anapowasili shuleni. Cheti hicho kiwe kimetolewa na daktari toka hospitali ya serikali au kutoka hospitali nyingine inayotambuliwa na serikali.

15. Kila mwanafunzi azingatie tarehe ya kufungua shule, endapo hatafika tarehe hiyo hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa au kutopokelewa kabisa.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vitu kama redio, cassette, kamera, simu ya mkononi, jiko la kupikia, hita na pasi akiwa shuleni akikamatwa navyo atafukuzwa shule mara moja.
17. Bidii katika masomo ndilo lengo mahususi kwa kila mwanafunzi. Kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu wastani wa**alama 50%** ifikapo mwisho wa mwaka, pungufu ya alama hizo mwanafunzi hataruhusiwa kuingia kidato kingine. Aidha kabla ya mtihani wa mwisho wa mwaka ufaulu chini ya wastani wa **50%** atakabiliwa na changamoto nzito.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na fedha bwenini zaidi ya **Tsh. 10,000/=** zinazozidi zitatunzwa katika ofisi ya mhasibu wa shule vinginevyo shule haitahusika na malalamiko yoyote.
19. Hakuna ruksa ya kuja kusalimia/kuonana na mtoto muda wote wa masomo mpaka kipindi cha likizo, isipokuwa ni ruksa mzazi kufika shuleni kuleta mahitaji kwa mawasiliano na ofisi tu, hii ni kuepuka kuathiri saikolojia ya kujifunza kwa watoto. Kwa matatizo zaidi uongozi wa shule utakujulisha kufika shuleni kwa ushauri.(**NO VISITING DAY**)
20. Lugha ya mawasiliano mwanafunzi awapo shuleni muda wote nje na darasani ni kiingereza tu, vinginevyo atakabiliwa na changamoto kali.

**MIMI MWANAFUNZI ……………………………………………………………..NAKIRI KUKUBALI KUSOMA MASOMO KATIKA MCHEPUO (COMBINATION) WA…………… NAKIRI KWAMBA; NIMESOMA NA KUZIELEWA KANUNI NA SHERIA ZA SHULE, HIVYO NINAAHIDI KUTII NA KUTEKELEZA KILA MOJA KAMA ZILIVYO AINISHWAHAPO JUU NA MAAGIZO YANAYOTOLEWA NA UONGOZI WA SHULE**.

**JINA LA MWANAFUNZI ……..……………………………………… KIDATO CHA ………..**
**SAHIHI ………..…………………………………….**
**JINA LA MZAZI/MLEZI ………………...………………………… SAHIHI………...…….**
**NAMBA YA SIMU ……………………………………………………………………………..**

## <u>MAONI YA MKUU WA SHULE:</u>

**…………………………………………………………………………………………………………**
**………………………………………………………………………………………………………**
**JINA LA MKUU WA SHULE………………………………………………… SAHIHI ……………..**

**“MUNGU AKUBARIKI/AWABARIKI” KARIBUNI SANA.**